# HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA PWANI -TUMBI

# JARIDA -TUMBI RRH

**APRIL - JUNI 2025** **TOLEO LA PILI**



Dkt. Amaani K. Malima

***Kutoka kwa Mwenyekiti,***
Kwa furaha kubwa napenda kuwakaribisha kusoma Jarida letu likiwa ni toleo la pili la mwaka 2025.Jarida hili ni Toleo la pili katika machapisho ya Jarida la Tumbi ambalo linawapa wasomaji wetu fursa ya kusoma makala mbalimbali za kuelimisha na kufurahisha zinazohusu shughuli zinazofanywa na hospitali.
Kwa kiwango kikubwa Jarida letu linaangazia shughuli za hivi karibuni zilizofanyika katika kipindi cha Machi - June 2025.

Pamoja na jarida hili hospitali ina tovuti (www.tumbirrh.go.tz),kurasa za mitandao ya kijamii ya facebook, X,pamoja na instagram (hospitali_ya_tumbi),ambazo ni zana mpya, zinazobadilisha mwelekeo wa utoaji na usomaj wa taarifa zetu,na zina umuhimu mkubwa katika kuwaweka karibu wadau wetu.Mwaka huu, tukiwa pamoja na wewe msomaji wetu, tunatarajia kuongeza wafuasi kwenye mitandao ya kijamii ya facebook, instagram, na kuifanya kuwa bora zaidi. Maoni yako, michango na ukosoaji wa kujenga juu ya yote uliyosoma katika jarida letu yamethibitisha kuwa na maana katika kutimiza dhamira yetu ya kutoa na kutengeneza jukwaa bora la habari.
Tunatumaini utaendelea kufurahia makala mbalimbali zinazotoka katika jarida hili.Wafanyakazi wetu na wahariri wataendelea kufanya kazi kwa utii na bidii katika kukuletea habari zinazohusu shughuli zote zinazofanywa na hospitali.

## TIMU YA WAHARIRI

**Dkt.Silas Msangi - Mwenyekiti**
**Abdulkarim R. Mussa - Mjumbe**
**Rosena Suka - Katibu**
**Florence A. Shahanga - Msanifu**

*Motto: Your health, our piority*
*“Afya yako, kipaumbele chetu"*

# JARIDA -TUMBI RRH

**APRIL - JUNI 2025** **TOLEO LA PILI**

**‘SERIKALI YA AWAMU YA SITA IMEENDELEA NA MABORESHO YA MIUNDOMBINU, WATAALAMU NA VIFAATIBA VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA IKIWA NI PAMOJA NA UJENZI WA MAJENGO MAPYA NA VIFAA VYA KISASA’.**



**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**

**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

Huduma za Kibingwa na Bobezi, Uchujaji wa Damu (Dialysis), Vipimo vya Radiolojia, Upatikanaji wa Dawa kwa zaidi ya wastani wa asilimia 96%, Kuimarika kwa Huduma za Matibabu, Uchunguzi wa Maabara.

## HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA PWANI -TUMBI


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**
**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA PWANI TUMBI**
S L P: 30041 Kibaha -Pwani, Simu: 0765 106 096
Barua pepe: barua@tumbirrh.go.tz
Tovuti: www.tumbirrh.go.tz


*“Afya yako, kipaumbele chetu"*

# JARIDA -TUMBI RRH

**APRIL - JUNI 2025** **TOLEO LA PILI**

## MWENGE WA UHURU WAZINDUA MRADI KISIMA CHA MAJI SAFI HOSPITALI YA TUMBI



Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2025, Ndugu Ismail Ally Ussi tarehe 02 Machi amezindua rasmi Kisima cha Maji Safi katika Hospitali ya Tumbi. Kisima hiki kina uwezo wa kuhifadhi maji zaidi ya lita laki tatu na kumi elfu (310,000), kitasaidia Hospitali kwenye upatikanaji wa maji safi na salama kwaajili ya huduma mbalimbali.







# JARIDA -TUMBI RRH

APRILI - JUNI 2025 TOLEO LA PILI


## WATUMISHI WA TBC WATOA MSAADA WA MAHITAJI KWA WATOTO NJITI TUMBI

Kikundi cha Misaada kutoka Shirika la Utangazaji Tanzania Broadcasting Corporation (TBC) , "MIKONO YA WANA". Tarehe 09 Aprili 2025, kimetoa msaada wa mahitaji mbalimbali muhimu kwa wakina mama waliojifungua watoto njiti katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani - Tumbi. MIKONO YA WANA ni kikundi kinachojumuisha watumsihi wa kada mbalimbali kutoka TBC, kwa niaba ya wenzao kimewashika mkono wa mama hawa kwa kutoa vitu mbalimbali kama sabuni, pampasi, mafuta ya nywele, sukari na pesa taslimu kwa ajili ya kununulia dawa.










# JARIDA -TUMBI RRH

**APRILI - JUNI 2025** **TOLEO LA PILI**

## WATUMISHI WA TBC WATOA MSAADA WA MAHITAJI KWA WATOTO NJITI TUMBI










# JARIDA - TUMBI RRH

APRILI - JUNI 2025 TOLEO LA PILI

## MAADHIMISHO YA SHEREHE ZA MEI MOSI 2025






Watumishi wa Hospitali ya Rufaa ya mkoa wa Pwani - Tumbi wameungana na Wafanyakazi kutoka katika Taasisi za Serikali na za Watu Binafsi za Mkoa wa Pwani kusheherekea Maadhimisho ya Siku Ya Wafanyakazi Duniani (MEI MOSI).

**KAULI MBIU YA MEI MOSI 2025** : *"Uchaguzi Mkuu wa 2025 utuletee Viongozi wanaojali na Kuthamini Haki na Masilahi ya Wafanyakazi sote tushiriki"*





# MAADHIMISHO YA SHEREHE ZA MEI MOSI 2025





*Kimkoa wa Pwani Maadhimisho haya yamefanyika katika Viwanja vya Shirika La Elimu Kibaha. Mgeni Rasmi katika Maadhimisho hayo alikua ni Mkuu wa Mkoa wa Pwani Mhe. Abubakar Kunenge.*







# WACHUNGAJI NA WANAKWAYA WA KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI K.K.K.T JIMBO LA MAGHARIBI DAYOSISI YA MASHARIKI NA PWANI WATOA MSAADA KWA WAGONJWA TUMBI



Wachungaji na Waimbaji wa Kwaya za Uinjilisti na Uamsho za Kanisa la Kiinjili La Kilutheri Jimbo la Magharibi, Dayosisi ya Mashariki na Pwani tarehe 11 Aprili 2025 wametoa Misaada kwa wagonwa waliopo kwenye Wodi mbalimbali za Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani Tumbi ikiwa ni sehemu ya kuonesha Matendo ya Huruma kwa wenye uhitaji.









# JARIDA -TUMBI RRH

**APRILI - JUNI 2025** **TOLEO LA PILI**

## WACHUNGAJI NA WANAKWAYA WA KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI K.K.K.T JIMBO LA MAGHARIBI DAYOSISI YA MASHARIKI NA PWANI WATOA MSAADA KWA WAGONJWA TUMBI












www.tumbirrh.go.tz hospitali_ya_Tumbi Kibaha

# MAADHIMISHO YA SIKU YA WAKUNGA DUNIANI





Kaimu Mganga Mkuu wa Hospitali ya Tumbi Dkt. Adam Gembe amekata keki na Wakunga pamoja na Wamama waliojifungua na wanaokaribia kujifungua katika kuadhimisha Siku ya Wakunga Duniani ambayo huadhimishwa kila tarehe 5 Mei 2025 duniani kote , ikiwa ni ishara ya Upendo na kuwatia moyo wakunga hao katika kuzidi kutoa huduma iliyo bora na kwa wakati sahihi.







## MAADHIMISHO YA SIKU YA WAKUNGA DUNIANI





# SHEREHE ZA SIKU YA WAUGUZI DUNIANI TAWI LA TUMBI

Maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani kwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani – Tumbi yaliadhimishwa tarehe 30 Mei 2025. Katika Ukumbi wa B. Merlin uliopo katika majengo ya Shirika la Elimu Kibaha. Mgeni rasmi katika maadhimisho haya alikua ni Mganga Mkuu wa Mkoa, Dkt. Kusirye Ukio kwa niaba ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Pwani Rashid Mchata.

Dkt. Kusirye Ukio katika hotuba yake aliwapongeza na kuwaasa wauguzi hao kwa kusema kwamba sekta ya Afya inayofanya shughuli za kinga na tiba asilimia kubwa ni nguvu ya Wauguzi, kwahiyo kauli mbiu ya mwaka huu tunaamini kwamba Wauguzi wakibaki ndani ya maadili ya taaluma yao na maadili ya utumishi, kada zote za Afya wataenda kubadilika kwa kutoa huduma bora kwa mteja.







Kwa upande wake Mganga Mfawidhi Dkt. Amaan Malima amesema kwamba Siku ya Wauguzi Duniani ni siku muhimu Duniani kote ambapo wanatambua, kuthamini mchango mkubwa wanaotoa Wauguzi katika kutoa huduma. Ameongezea kuwa kauli mbiu ya mwaka huu isemayo "Uuguzi Nguvu ya Mabadiliko" inaakisi mchango mkubwa unaotolewa na Wauguzi na kuwataka waendelee kuzingatia maadili ya taaluma yao.







## SHEREHE ZA SIKU YA WAUGUZI DUNIANI TAWI LA TUMBI



Maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani huadhimishwa kila ifikapo tarehe 12 Mei kila mwaka. Lakini kutokana na mwingiliano wa kazi Wauguzi wa Mkoa wa Pwani wamefanya maadhimisho hayo Mei 30 2025.



# SIKU YA MAGONJWA YA DHARURA NA AJALI DUNIANI (WORLD EMERGENCY DAY)




Idara ya Magonjwa ya Dharura na Ajali (EMD), wameungana na wenzao Duniani kote Kuadhimisha Siku ya Magonjwa ya Dharura na Ajali Duniani(WORLD EMERGENCY DAY), ambayo ni tarehe 27 Mei kila mwaka, kwa kusheherekea pamoja siku hii muhimu kwa lengo la kuzidi kuwatia moyo wataalamu wa tiba hizi za ajali na dharura na kuhimiza ushirikiano kwa kutoa huduma bora. ***KAULI MBIU 2025 :*** *“Sisi Wataalamu wa Tiba za Dharura na Ajali tunajivunia kutoa Huduma za Dharura”.*









# KIKUNDI CHA KIKOBA CHA WOMEN OF HOPE CHA TOA MSAADA TUMBI




Kikundi cha Kikoba cha Wanawake wa Kibamba (WOMEN OF HOPE) wakiwa na baadhi ya Watumishi wa KItengo cha Ustawi wa Jamii cha Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani Tumbi walipokuja kutoa msada wa mahitaji mbalimbali kwa watoto wachanga waliozaliwa na watoto waliolazwa kwenye wadi za watoto Hospitalini hapa Tumbi.









# TAASISI YA KOFIH YATEMBELEA HOSPITALI YA TUMBI

Timu ya watu saba kutoka taasisi ya Korea Foundation for International Healthcare (KOFIH) wametembelea Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani – Tumbi tarehe 24 Juni, 2025. Lengo la Timu hii ni kufuatilia miradi iliyofadhiliwa na taasisi hiyo na kujua shughuli mbalimbali za Hospitali zinavyoendeshwa. KOFIH iliwezesha hospitali ya Tumbi kupatiwa mashine na vifaatiba mbalimbali ambavyo vimekuwa msaada mkubwa katika utoaji wa huduma mbalimbali za afya.






Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mkoa wa Pwani – Tumbi, Dkt. Amaan Malima, aliishukuru Taasisi ya KOFIH pamoja na Serikali ya Korea kwa misaada ya vifaatiba mbalimbali waliyoitoa kwa Hospitali kwa kusema vifaatiba hivyo vinasaidia s katika kutoa huduma mbalimbali za afya kwa wananchi.

Maeneo ambayo Taasisi hiyo walifadhili ni eneo la afya katika huduma za wajawazito na uzazi, watoto wachanga, mashine ya kutakasa vifaatiba, ununuzi wa jenereta la kisasa, ununuzi wa mashine ya ufuaji nguo pamoja na upanuzi wa jengo la watoto waliochini ya uangalizi maalum.

# TAASISI YA KOFIH YATEMBELEA HOSPITALI YA TUMBI





Timu iliokuwepo kwenye msafara huo ni Bwn. Changi Ho Lee (CEO,GCK Co., Ltd Director, Global Together), Prof. Sunjoo Kang, Gyeongbae Seo (Mwakilishi wa KOFIH Tanzania), Bwn. Joonhyoung An ( Vice President, STN sports TV/News), Dkt.Yoo Rha Hong (Neonatologist, Associate Professor, Department of Pediatrics, Kosin University College of Medicine), Prof. Jee Young Lee (Assistant Professor, Department of Microbiology, Kosin University College of Medicine) na Bi. Josephine Kingi (Msimamizi wa Ofisi KOFIH Tanzania.





# JARIDA -TUMBI RRH

APRILI - JUNI 2025

TOLEO LA PILI



MHE. JENISTER MHAGAMA
WAZIRI WA AFYA



DKT. GODWIN MOLLEL
NAIBU WAZIRI

"Afya yako ,kipaumbele chetu".

KARIBUNI KWA HUDUMA ZA UCHUNGUZI, USHAURI NA MATIBABU

TUNAPATIKANA KIBAHA MJI,PWANI

HUDUMA ZETU NI SAA 24 KILA SIKU,
TUNAPOKEA BIMA ZA AFYA ZIKIWEMO NHIF, STATEGIES, JUBILEE, ICHF